JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

Anuani ya simu:- MKUU WA SHULE

Simu:- 0756281490 au 0762024346

Email: makogasecondary@gmail.com

(Mawasiliano yote ya kiofisi yaandikwe

Kwa mkuu wa shule na sio mtu binafsi)

SHULE YA SEKONDARI MAKOGA,

S.L.P 230,

NJOMBE

18/ 06/2018

Unapojibu tafadhari taja

KUMBU. NA. MAKO/SS/ED/A.VOL I/I

Ndugu…….

Mzazi/mlezi……....

……

YAH: KUCHAGULIWA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO MWAKA 2018

Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika shule hii mwaka 2018 tahasusi ya…… shule ya Sekondari Makoga ipo umbali wa kilometa thelathini na moja (31km) Magharibi mwa mji wa Njombe, usafiri wa Basi na Noa ni Tsh 3000/= toka kituo cha mabasi hadi shule ilipo.

Muhula wa kwanza wa masomo unaanza tarehe 16/07/2018 hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe 15/07/2018 mwisho wa kuripoti ni tarehe 30/07/2018.

2. KAULI MBIU YA SHULE 'SCHOOL MOTTO' ELIMU NI UFUNGUO WA MAFANIKIO.

Kauli hiyo ndiyo dira yako utakapo kuwa hapa kwa kipindi chote cha miaka miwili. Unatakiwa kuitafakari kauli hiyo kwa vitendo. Ni matumaini yetu kuwa utatumia nafasi hii adimu kwa manufaa yako na kwa taifa kwa ujumla. Hivyo basi, utatakiwa kuwa na tabia njema na uhudhurie masomo na ujifunze kwa bidii.

……

E.T.MLOWE

MKUU WA SHULE

2.2. ADA NA MICHANGO MINGINE YA SHULE

(a) Ada ya shule kwa mwaka ni shilingi 70,000/= mwanafunzi atalipa shilingi elfu 35,000/= kwa muhula kupitia akaunti namba **60601000015 NMB** jina la akunti ni MAKOGA SECONDARY SCHOOL. Tafadhari andika jina la mwanafunzi na mchepuo wake kwenye pay in slip. Pindi afikapo shuleni aiwsilishe kwa mhasibu wa shule.

(b) Michango mingine inayotakiwa kulipwa na kila mzazi ni:-

(i) 15,000/= kwa ajili ya ukarabati wa samani

(ii) 6,000/= kwa ajili ya kitambulisho

(iii) 20,000/= kwa ajili ya taaluma (kwa mwaka)

(iv) 30,000/= kwa ajili ya kulipa wapishi, walinzi na vibarua wengine (kwa mwaka)

(v) 10,000/= kwa ajili ya huduma ya kwanza

(vi) 5,000/= tahadhari (haitarejeshwa)

(vii) 2000/= nembo ya shule.

Juma ya Ada na michango mingine ni Tsh. 158,000/=

(c) Mahitaji muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuleta shuleni ni:-

(i) Ream ya karatasi 1 ya A4 nyeupe (kwa mwaka)

(ii) Vitabu vya masomo ya tahasusi husika (orodha imeambatanishwa)

(iii) Dissecting kit kwa mwanafunzi wa biology

(iv) Scientific calculator

(v) Godoro moja la futi 3x6 nchi 4 Dodoma

(vi) Mashuka pair 2 (bluu), blanketi 1, foronya 1, chandarua 1

(vii) Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe)

(viii) Aje na ndala za kuogea

SARE YA SHULE: WAVULANA

- Suruali mbili (2) za shule rangi ya Dark Blue zenye mifuko miwili (2) mbele na mmoja (1) nyuma. Upana miguuni inchi 18. Iwe na linda mbili (2) kila upande (dats)
- T-shirt (2) za kijivu (shamba dress)
- Sweta mbili (2) rangi ya kijivu
- Makoga ni baridi sana mwanao aje na track suit rangi ya kijivu, isiwe na kofia.
- Mashati meupe mawili ya mikono mirefu
- Tai moja dark blue
- Viatu vya ngozi nyeusi na visivyo na visigino virefu jozi mbili vya kufunga na kamba.
- Soksi jozi mbili nyeusi
- Raba na nguo za michezo (rangi nyekundu au kijani)

- Koti jeupe lenye mikono mirefu (laboratory coat) kwa wanafunzi wanao soma masomo ya sayansi tu.
- Suruali maruni mbili (2) za kitambaa, sare ya kazi za nje ya darasa mshono wa suruali:- iwe na mifuko mitatu, mmoja wa nyuma upande wa kulia na miwili mbele pande zote kulia na kushoto pembeni, iwe na linda mbili kila upande upindo wa chini (miguuni) ugeuzwe juu (turn up) upana miguuni inchi 18 tu na si vinginevyo.
- Jacketi jeusi moja lisilo na mfuniko kujikinga na baridi.

NB: Suruali za mitumba na jeans haziruhusiwi hapa shuleni. Mwanafunzi anapokuja shuleni awe amevaa tracksuit na T-shirt ya kijivu, zilizo agizwa hapo juu.

SARE YA SHULE: WASICHANA

- Sketi mbili (2) Dark Blue, zenye rinda box , sketi ziwe ndefu zinazofika usawa wa kisigino.
- Gauni mbili (2) mshono wa solo mikono mifupi rangi ya Maruni ya udongo (shamba dress).
- Sweta mbili (2) rangi ya kijivu
- Makoga ni baridi sana mwanao aje na tracksuit rangi ya kijivu na isiwe na kofia.
- Mashati meupe mawili ya mikono mirefu
- Tai moja dark blue
- Viatu vya ngozi vyeusi na visivyo na visigino virefu jozi mbili vya kufunga na kamba.
- Soksi jozi mbili nyeupe
- Raba na nguo za michezo (rangi nyekundu au kijani)
- T-shirt (2) za kijivu (shamba dress)
- Koti jeupe lenye mikono mirefu (laboratory coat) kwa wanafunzi wanao soma masomo ya sayansi tu.
- Blanketi ndogo 2
- Night dress 2 nyeupe
- Taulo
- Jozi moja ya kitenge
- Kwa waislam waje na hijabu nyeupe zinazofunika mabega.
- Jacketi jeusi moja lisilo na mfuniko kujikinga na baridi.

VIFAA VINGINE VINANYOHITAJIKA SHULENI:-

i. Wavulana waje na jembe lenye mpini na hardbloom moja kwa ajili ya usafi.
ii. Wasichana waje na mopa moja na panga moja
iii. Ndoo mbili moja ndogo lita 10 kwa matumizi ya mwanafunzi mwenyewe na nyingine lita 20 kwa matumizi ya ofisi shuleni. Kwa wanafunzi wa kiislamu wanatakiwa kuja na ndoo tatu, ndoo mbili kwaajili ya matumizi ya mwanafunzi mwenyewe na moja kwa matumizi ya ofisi ya shuleni.
iv. Madaftri makubwa kumi (10) aina ya 'COUNTER BOOK' na kalamu za kutosha, mkebe na scientific calculator fx 991 kwa wanafunzi wote.
v. Toilet papers za kutosha (12-15) kwa mhula mmoja.
vi. Vitabu vya masomo angalia orodha iliyoambatanishwa kwa kila somo. Anaweza kununua baadhi ya hivyo.

MASHARTI MENGINE

- Mwanafunzi asije na nguo nyingine zaidi ya zile alizoagizwa vinginevyo atarudishwa nyumbani.
- Kila mwanafunzi anatakiwa kuwa mlinzi wa mwenzake kuzuia uovu unaoweza kutokea katika chumba chao. Uharibifu wowote ule ukitokea/ukibainika katika chumba kimojawapo wanafunzi wanaoishi katika chumba hicho wataadhibiwa wote, kwani wote watakuwa wameshiriki katika uharibifu wa mali ya umma. Mfano kuunganisha umeme, kuchoma bweni, kuiba vitu, nk.
- Uharibifu wowote utakao sababishwa na mwanafunzi ni jukumu la mwanafunzi au mzazi/mlezi kugharamia matengenezo.

MAWSILISNO TOKA KWA MZAZI:

Maagizo yote ya mizigo yatumwe posta tu, ambapo muhudumu wa shule anaweza kuchukua na kuleta shuleni. Mwanafunzi hata ruhusiwa kwenda kuchukua. Aidha taarifa nyingine inayomhusu mwanafunzi mfano taarifa ya kufiwa itumwe kwa mkuu wa shule na si kupitia kwa mwanafunzi. Taarifa kama hiyo haita sikilizwa.

USAFI BINAFSI:

Unatakiwa kuja shuleni na nywele fupi, usinyoe panki au upara, hairuhusiwi kufuga ndevu wala kucha wala kupaka rangi kwenye kucha, usije na vipodozi. Aidha unatakiwa kuwa safi na uoge mara kwa mara.

UTUNZAJI WA MAZINGIRA NA USAFI:

Unatakiwa utunze mazingira ya shule katika hali ya ubora na usafi.

USHIRIKI KATIKA KAZI ZA MIKONO:

Ni wajibu wa kila mwanafunzi kushiriki kazi za mikono ambazo zina lengo la kuendeleza Elimu ya Kujitegemea pamoja na kuimarisha afya ya mwili.

NIDHAMU:

Ili uweze kujifunza na kufaulu katika masomo yako unatakiwa kuwa na nidhamu ya hali ya juu. Unatakiwa kuzisoma na kuzielewa vizuri sheria za shule zilizo ambatanishwa nyuma ya fomu hii. Pia ifahamike kuwa si jukumu la shule kutoa nauli pindi mwanafunzi anapopatikana na makosa ya kinidhamu ya kumrudisha nyumbani. Ni wajibu wako mzazi au mlezi.

MICHEZO NA UTAMADUNI:

Unatakiwa kushiriki michezo na utamaduni kwa lengo la kuleta uhusiano mwema na kujenga miili yenye afya. Jitokeze na ibua kipaji chako katika fani mablimbali mfano kuimba, kuigiza, skauti na kadhalika.

DINI:

Kila mwanafunzi anaruhusiwa kufanya ibada kulingana na imani yake ili mradi shughuli hizo zinaendeshwa kwa kufuata sheria za nchi na ratiba ya shule. Aidha mwanafunzi atasali/swali shuleni na maeneo yaliyo karibu na shule.

CHAKULA MAALUMU:

Shule haitatoa chakula maalumu kwa wanafunzi tofauti na wengine.

Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu. Nakutakia maandalizi mema na safri njema ya kuja Makoga sekondari.

Karibu sana.

MKUU WA SHULE

Nakala kwa:-

1. Katibu
   Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa
   S.L.P 1923
   DODOMA

2. Katibu Tawala Mkoa
   S.L.P 668,
   NJOMBE.

3. Mkurugenzi Mtendaji Wanging'ombe
   S.L.P 64,
   NJOMBE.

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

MAELEZO BINAFSI YAHUSUYO MWANAFUNZI

A.

1. Jina la mwanafunzi .....
2. Tarehe ya kuzaliwa .....
3. Mahali alipozaliwa (Wilaya) ..... (Mkoa).....
4. Dini ..... Dhehebu .....

B.

1. Jina la mzazi/mlezi anayekutunza .....
2. Kazi ya mzazi/mlezi .....
3. Anuani ya mzazi/mlezi.....
4. Mahali anapoishi mzazi/mlezi.....
   Kijiji/mji ..... Kata .....
5. Jina la anayekulipia Ada /Karo ya shule .....
6. Anuani yake .....
7. Namba ya simu .....

C. Majina ya ndugu wengine wawili wanohusika na malezi ya mwanafunzi huyo. Ingalifaa wawe wanaoishi Njombe au karibu na Njombe kwa ajili ya mawasiliano ya haraka.

1. Ndugu .....
   Anwani yake.....
   Namba ya simu .....
2. Ndugu .....
   Anwani yake.....
   Namba ya simu .....

D:- Anuani za ofisi ya mtendaji kata au mwenyekiti wa mtaa/kijiji ambako mzazi/mlezi wa mwanafunzi anaishi.

1. Jina la mtendaji kata .....
   Anwani yake.....
   Namba ya simu .....
2. Jina la mwenyekiti wa mtaa/ kijiji.....
   Anwani yake.....
   Namba ya simu .....

- Zingatia: Tafadhali ijaze fomu hii kwa uangalifu.

- Futa isiyohusika.

KIAPO CHA MWANAFUNZI

Jina la mwanafunzi .....

Anuani .....

Tarehe .....

Mimi .....nimesoma maagizo ya shule ya sekondari Makoga kwa makini na kuyaelewa. Naahidi kuwa mwanafunzi mtiifu nitazingatia sheria, taratibu za shule kama nitakavyoelekezwa.

KIAPO CHA MZAZI/MLEZI

Mimi ..... mzazi/mlezi wa ..... nimesoma kwa makini maagizo ya shule yaliyotolewa yanayomhusu mtoto wangu. Ninakubali kuwa mwanangu achukue nafasi hiyo. Ninaahidi pia kuwa nitashirikiana na uongozi wa shule katika kumkuza na kumlea mwanafunzi huyu kielimu na kitabia.

Sahihi ya mzazi/mlezi.....

Tarehe .....

GOVERNMENT OF TANZANIA

REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION

The headmaster,

Makoga Secondary School,

P.O. Box 230,

NJOMBE.

Part A:-

To Medical Officer

.....

.....

Mr/Mrs/Miss.....

(Name in Full)

Please examine the above named as to his/her physical and mental fitness for a full time schooling course. The examinations should include the following categories (1-3) each category or sub-category of which will render the applicant in eligible in case of a defect.

1.
    a.) Eye-sight.....
    b.) Hearing.....
    c.) Limbs.....
    d.) Speech.....
    e.) Venereal diseases.....
    f.) Leprosy.....
    g.) Epilepsy.....
2. Neuroses.....
3. Other serious diseases.....

Part B:- MEDICAL CERTIFICATE

(To be completed by government medical officer)

I have examined the above name and consider that he/she is physically fit/unfit mentally fit/unfit for a full time schooling course.

Date ..... Signature .....

Station ..... Designation .....

ORODHA YA BAADHI YA VITABU KWA KILA SOMO:-

A: HISTORY

1. Modern World History (Ben Walsh).
2. Africa in the World History (Nyirenda).
3. The Russian Revolution and the Bolshevic Victory (D.C. Heath and Company).
4. Major Events in the African History (Fr. Kamara).

B: CHEMISTRY

1. Advanced Chemistry Review (William W. Davis: Mzumbe bookshop project, 2004).
2. Physical Chemistry (Delungu et al: Mzumbe bookshop project, 1998).
3. Advanced Level Inorganic Chemisty part I and II (Tanzania Institute of education, 1995).
4. Organic Chemistry vol. I. The Fundamental Principles (I.L. Finar , Longman Ltd. 1990).

C: KISWAHILI

1. Kunga za Fasihi na Lugha (Msokile M. 1992. EDP.
2. Historia ya Kiswahili Africa Mashariki (Shiraghdin na Mnyampala).
3. Kunga za Ushairi na Diwani Yetu (Mlokozi M. na K.K. Kahigi 1982 TPH).
4. Sarufi ya Kiswahili Sekondari na Vyuo (Mdee., DUP-DSM.
5. Ndimi na Hisi za Wahakiki katika Kioo Cha Lugha-DSM (Senkoro 1973).
6. Kamusi ya Kiswahili Sanifu-TUKI

D: GEOGRAPHY

1. Principle of Physical Geography (F. J. Monkhouse).
2. Geography, Integrated Approach (D. Waugh).
3. Practical Geography for Africa (J. M. Pritchard).
4. General Geography in diagram. (R.B. Bunnert).
5. Simplified Physical Geography (A-Level, D.M. Mapunda).
6. Statistical Methods and the Geographer. (S. Gregory).
7. Certificate physical and Human Geography (Goh Chang Leong).

E:- BIOLOGY

1. New Understanding Biology (Suzan Toole).
2. Advanced Biology principles and Application (C.J. Clegg and D.G. Mackean).
3. Advanced Biology (Michael Kent)
4. Dissecting Kit

SHERIA ZA SHULE YA SEKONDARI MAKOGA

1. Mwanafunzi anatakiwa kusimama kumsalimia mtu yeyote anayemzidi umri wakati wote na mahali pote.
2. Mwanafunzi anatakiwa kuheshimiana na kushirikiana na wenzake.
3. Mwanafunzi anatikiwa kuheshimu na kufanya kazi anazopewa.
4. Mwanafunzi anatakiwa kuheshimu bendera ya taifa, wimbo wa taifa, fedha ya taifa wakati wote.
5. Mwanafunzi anatakiwa kuwa msafi na kutunza mazingira vizuri.
6. Mwanafunzi awapo shuleni alale katika bweni husika pekee.
7. Mwanafunzi anatakiwa kuwa mfano mwema ndani na nje ya shule.
8. Mwanafunzi anatakiwa kuheshimu ofisi ya mkuu wa shule, ofisi zote za shule, ukumbi wa chakula, maktaba na madarasa.
9. Mwanafunzi anatakiwa kuhudhuria masomo yote kwa wakati na kumfanya mitihani inayomhusu.
10. Mwanafunzi anatakiwa kuhudhuria mikutano yote shuleni kama vile: kupandisha bendera ya taifa, baraza la shule, mikutano ya bweni, darasa, nk.
11. Mwanafunzi anatakiwa kutii kengele kama mwito wa haraka.
12. Mwanafunzi anatakiwa kuvaa sare ya shule.
    a.) Darasani
    b.) Anapotoka nje ya shule
    c.) Wakati wa baraza la shule
13. Mwanafunzi atatoka nje ya shule kwa ruhusa maalumu ya:
    a.) Mwalimu wa zamu na kuwepo shuleni kabla ya saa 12 kamili jioni.
    b.) Mkuu wa shule tu kwa kibali cha kulala nje ya shule.

NB: Mwanafunzi akilala nje ya shule bila ruhusa atukuwa amejifukuzisha shule mwenyewe.

14. Mwanafunzi haruhusiwi kutembelea nyumba za walimu na watumishi wengine ila kwa kibali maalumu tu. Sehemu hizi ni nje ya mipaka ya shule.
15. Mwanafunzi haruhusiwi kuingiza mgeni yeyote bwenini au darasani.
16. Mwanafunzi haruhusiwi kutembelea au kujihusisha na maeneo yafuatayo:-
    a.) Vilabu vya pombe
    b.) Majumba ya kufikia wageni (Guest Houses).
17. Mwanafunzi anatakiwa kutunza mali binafsi pamoja na mali za umma kama vile madawati vitanda, vifaa vya chakula, vitabu na vifaa vya maaabara pamoja na majengo yote ya shule.
18. Mwanafunzi haruhusiwi kwa namna yoyote kumiliki au kutumia vifaa vinavyotumia umeme awapo shuleni kama vile:
    a.) SIMU
    b.) JIKO
    c.) HEATER
    d.) REDIO

MAKOSA YANAYOWEZA KUSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE

1. Wizi
2. Uasherati, ubakaji na ushoga
3. Uvutaji bangi
4. Kupigana au kumpiga mwalimu au mtumishi
5. Kuoa au kuolewa
6. Kupata au sababisha mimba ndani na nje ya shule
7. Kutoa mimba
8. Kutoa lugha chafu au ya matusi.
9. Kupatikana na makosa ya jinai
10. Kugoma, kuchochea au kuongoza migomo shuleni
11. Kukataa adhabu halali kwa makusudi
12. Kupatikana na simu au vifaa vya simu.